

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KAZI NA AJIRA

Anuani ya simu: "KAZIMKOA"
Simu:
Fax: **2112054**
Barua pepe: kazi@africaonline.co.tz



IDARA YA USIMAMIZI WA KAZI
NA HUDUMA ZA UKAGUZI

S.L.P. 1181

DAR ES SALAAM.

28/10/2011

Kumb. Na.DAR/10/5/53/52

Unapojibu tafadhali taja:

Mwenyekiti/Katibu,
Chama cha Wamiliki wa Magari ya Mizigo Tanzania (TATOA)
DAR ES SALAAM - Aione Ndugu Hans-pope.

Mwenyekiti/Katibu,
Chama cha Wamiliki wa Magari ya Abiria (Mabasi) Tanzania
(TABOA),
DAR ES SALAAM - Aione Ndugu Mohamed Hood.

Mwenyekiti/Katibu,
Chama cha Wamiliki wa Magari ya Abiria (Daladala) Mkoa wa
Dar es Salaam (DARCOBOA),
DAR ES SALAAM - Aione Ndugu Sabri Mabruki.

Mwenyekiti/Katibu,
Chama cha Wamiliki wa Magari ya Abiria (Mabasi),
Mkoa wa Dar es Salaam (DARBOA).
DAR ES SALAAM - Aione Ndugu Severin Ngalo.



**YAH: UTEKELEZAJI WA SHERIA YA AJIRA NA MAHUSIANO
KAZINI NA.6 YA MWAKA 2004 – MIKATABA YA AJIRA**

Rejea somo tajwa hapo juu pamoja na Mkutano wa Wadau wa Sekta ya Usafirishaji uliofanyika tarehe 12 Oktoba, 2011 katika ukumbi wa Mikutano wa Wizara ya Kazi na Ajira, kuzungumzia suala la Mkataba wa Ajira, hususan Mkataba wa Ajira ya Madereva Nchini.

Pamoja na barua hii, nawatumia Taarifa/Muhtasari wa mkutano huo ambao uliazimia masuala kadhaa yanayohitaji utekelezaji wa haraka.

Kama mtakavyoona, Wadau pamoja na Madereva wamekubaliana kuwa Mkataba wa Ajira uliotayarishwa kwa mujibu wa Sheria iliyotajwa hapo juu ikisomwa pamoja na Tangazo la Serikali Na.42 la tarehe 16 February 2007, utumike kama ulivyo.

Wizara imeshatekeleza moja ya maazimio ya Mkutano huo kuhusu kutoa taarifa kwenye Vyombo vya Habari (Magazeti) juu ya kukubalika kutumika kwa Mkataba wa Ajira (Magazeti ya Mtanzania na Habari Leo ya tarehe 26/10/2011). Barua hii ni utekelezaji wa azimio lingine linalohitaji Wizara iwajulishe Wadau, hususani wamiliki wa Magari ya Abiria na Magari ya Mizigo kuhusu maazimio yaliyofikiwa na Mkutano huo.

Aidha, ninawatumia nakala mbili (2) ya Mkataba wa Ajira, moja kwa lugha ya Kiswahili na nyingine kwa lugha ya Kiingereza kwa ajili ya kujaza na kuwapatia nakala Madereva pamoja na wafanyakazi wengine mlionao. Ni vema picha ya mfanyakazi iwekwe/ibandikwe kwenye Mkataba wake wa Ajira.

Kama tulivyoeleza kwenye taarifa iliyotolewa kwenye Magazeti tajwa hapo juu, Wizara ya Kazi na Ajira kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Dola itaendelea na zoezi la kufanya ukaguzi kwa mwajiri mmoja mmoja kuona utekelezaji wa jambo hili na Sheria za Kazi kwa ujumla.

Ni matumaini yetu kuwa mtawapatia wanachama wenu (Wamiliki wa Magari ya Mizigo na Magari ya Abiria) taarifa hii na kuwahimiza kuzingatia Sheria, hususani Sheria za Kazi, ili kuboresha na kudumisha mahusiano mema kazini na kuongeza tija.


B.J. Mushi
Kny: KAMISHNA WA KAZI

- Nakala kwa: Mwenyekiti/Katibu,
Chama cha Madereva wa Malori Tanzania
(CHAMAMATA)
S.L.P. 62435,
DAR ES SALAAM - Kwa taarifa na ufuatiliaji wa suala hili.
- “ “ Mwenyekiti/Katibu,
Chama cha Madereva wa Malori na I.T (T.T.A.I.T.D.A.),
S.L.P. 16671,
DAR ES SALAAM - Kwa taarifa na ufuatiliaji wa suala hili.
- “ “ Katibu Mkuu,
Umoja wa Madereva wa Mabasi Tanzania
(UWAMATA),
S.L.P. 55633,
DAR ES SALAAM - Kwa taarifa na ufuatiliaji wa suala hili.
- “ “ Katibu Mkuu,
Umoja wa Madereva na Makondakta wa Mabasi ya Abiria (Daladala) Mkoa wa Dar es Salaam
(UWAMADAR),
S.L.P. 41264,
DAR ES SALAAM - Kwa taarifa na ufuatiliaji wa suala hili.
- “ “ Katibu Tawala (M),
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
S.L.P. 5429,
DAR ES SALAAM
- “ “ Katibu Mkuu,
Wizara ya Uchukuzi,
S.L.P. 9144,
DAR ES SALAAM - Kwa taarifa, barua yako ya tarehe 07/10/2011 Kumb.Na.CA 230/505 /01/103 yahusika.

“ “ Mkurugenzi Mkuu,
SUMATRA,
S.L.P. 3093,
DAR ES SALAAM - Pamoja na nakala ya Mkataba wa Ajira, rejea barua yetu ya tarehe 18/10/2011 Kumb.Na. DAR/10/5/82. Kama tulivyokubaliana, ni vema ukajiridhisha na Mkataba ambao mwajiri atauwasilisha kwako kabla ya kuendelea na taratibu za kumpatia Leseni.

“ “ Kamanda wa Polisi,
Kikosi cha Usalama Barabarani,
S.L.P. 1712,
DAR ES SALAAM - Pamoja na taarifa ya mkutano na nakala ya Mkataba. Tunaomba ushirikiano wako hususani uhakiki wa Mkataba wa Dereva husika wakati wa zoezi la Ukaguzi wa Magari linapofanyika Barabarani.

“ “ Katibu Mkuu,
COTWU (T),
S.L.P. 13920,
DAR ES SALAAM - Kwa taarifa.